

HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA

Subject: UGAVI

Error: IllegalOperatorSequence

Operator: Mchoko Comment

Namba: + 255 28 2690061

Namba ya Fax: + 255 28 2690061

E-mail: dedrorya@yahoo.com



OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI
KITENGO CHA UGAVI
S. L.P 250
RORYA - TARIME.

29/1/2019

TANGAZO

ZABUNI KWA WATOA HUDUMA MBALIMBALI KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA

Halmashauri ya Wilaya ya Rorya imetenga kiasi cha fedha katika bajeti yake ya mwaka wa fedha 2018/2019 kugharamia Shughuli mbalimbali za maendeleo. Aidha Halmashauri inakusudia pia Kuwapata wazabuni watakao toa huduma mbali mbali katika Halmashauri ya Wilaya ya Rorya. Bodi ya zabuni ya Halmashauri ya Wilaya ya Rorya chini ya utaratibu wa zabuni za kiushindani, Inawatangazia wananchi, makampuni, taasisi mbalimbali, Vikundi vilivyoandikishwa zabuni za kutoa huduma mbalimbali katika shule za sekondari na Msingi, Zahanati, na vituo vya Afya na Halmashauri ya Wilaya ya Rorya. Hivyo inawaalika wote kuomba zabuni zifuatazo kama zinavyoonyeshwa hapa chini.

- i. Zabuni ya vifaa vya Ujenzi Namba. LGA/068/2018/2019/G/01
- ii. Zabuni za vifaa vya Maabara na kemikali Zabuni LGA/068/2018/2019/G/02
- iii. Zabuni za uuzaji wa vitabu katika shule za msingi na sekondari LGA/068/2018/2019/G/03
- iv. Zabuni za Shajala, vifaa vya ofisi na usafi LGA/068/2018/2019/G/04
- v. Zabuni ya huduma ya chakula mashuleni LGA/068/2018/2019/G/05
- vi. Zabuni za Samani za ofisi na matengenezo ya madawati. LGA/068/2018/2019/G/06
- vii. Zabuni za Huduma za Kudurufisha (Printing services) LGA/068/2018/2019/NC/01

MASHARTI YA JUMLA YA ZABUNI

- (i) Zabuni ambazo hazitapokelewa na kusomwa hadharani siku ya ufunguzi wa Zabuni hazitafikiwa na Bodi ya zabuni ya Halmashauri kwa sababu yoyote ile.
- (ii) Vigezo vya tathmini ya zabuni zote vitakuwa kama vilivyoainishwa kwenye tangazo na kwenye nyaraka ya zabuni husika.
- (iii) Maombi yanatakiwa kutumwa kwenye bahasha iliyofungwa kwa lakiri na **kuonyesha zabuni iliyoombwa** bila kuwa na alama yoyote ya kuashiria ilikotoka na yatumwe kwa anwani ifuatayo:-
- (iv) Zabuni itanunuliwa kwa kiasi cha Sh.50,000/= ambayo haitorudishwa.

**Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya
S. L. P 250
RORYA**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 19/02/2019 saa nne asubuhi na zabuni zitafunguliwa hadharani mara tu siku na saa hiyo kuwadia kwenye ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Rorya. Waombaji au wawakilishi wao wanaalikwa kwenye zoezi la ufunguzi.

EXECUTIVE DIRECTOR
RORYA DISTRICT COUNCIL



MKURUGENZI MTENDAJI (W)

HALMASHAURI YA WILAYA

RORYA